HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

MPANGO WA USIMAMIZI MISITU

KIJIJI CHA NAINOKWE

UMEANDALIWA NA KAMATI YA MALIASILI YA KIJIJI CHA NAINOKWE

SEPTEMBA 2010

YALIYOMO

1 UTANGULIZI 4
1.1 Umiliki wa msitu 4
1.2 Lengo kuu la ya Mpango wa usimamizi wa misitu 4
1.3 Madhumuni 4
1.4 Mfumo wa Usimamizi 5
1.5 Muda 5

2 HISTORIA FUPI YA MPANGO 6
2.1 Jamii 6
2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii 6
2.2 Maelezo kuhusu Msitu 6
2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake 6
2.2.2 Vyanzo vya Maji 6
2.2.3 Hali ya Udongo 7
2.2.4 Uoto wa asili na Mazingira 7
2.2.5 Jamii za Miti ya Mbao 7
2.2.6 Mazao Yasiyotimbao 7
2.2.7 Wanyama Pori na Jamii za Mimea 7
2.3 Maeneo Madogo ya Usimamizi (EDU) 7
2.4 Matumizi ya Msitu 8
2.4.1 Mambo ya Asili na Haki za Kijadi 8
2.4.2 Historia ya Nyuma 8
2.4.3 Matumizi ya sasa 8

3 MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU 9
3.1 Matumizi ya msingi 9
3.2 Matumizi huru ya msitu 9
3.3 Shughuli katika msitu zitakazotozwa ushuru 9
3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji 9
3.4.1 Utaratibu wa kupata vibali ya uvunaji miti ya mbao 9
3.4.2 Mazao mengine ya misitu yatokanayo na leseni 10
3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu 10

4 HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU 11
4.1 Kijiji 11
4.1.1 Haki 11
4.1.2 Manufaa 11
4.1.3 Majukumu ya Halmashauri Kijiji 11
4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili 12
4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji 12
4.2 Halmashauri ya Wilaya 12
4.2.1 Haki 12
4.2.2 Manufaa 13
4.2.3 Majukumu 13
4.3 Serikali Kuu 13
4.3.1 Majukumu 13

5 SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU 14
5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu. 14
5.2 Ulinzi wa msitu 14
5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu. 14
5.2.2 Walinzi wa doria 14
5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Kuzuia Moto 14

6 MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU 15
6.1 Vyanzo vya mapato 15
6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau 15

6.3 Matumizi ya mapato 15
6.4 Ukusanyaji na utunzaji wa Fedha 15
6.4.1 Vitabu muhimu vya kutunza kumbukumbu vinavyotakiwa 16
6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi 16
6.4.3 Kuwajibishwa 16

7 UFUATILIAJI NA TATHIMINI 17

7.1 Ufuatiliaji 17
7.2 Tathimini ya kati na ya mwisho 17
Mpango wa Usimamizi Misitu 18
Marekebisho ya Mpango 18

KIAMBATISHO A – RAMANI YA MSITU WA KIJIJI 19

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Kijiji 19
Ramani Awali inayoonyesha Matumizi ya Ardhi ya Kijiji 20
Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji 20
Ramani ya Usawa kutoka Baharini ya Msitu wa Kijiji 22
Ramani Shirikishi ya Msitu wa Kijiji 22

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI 22

Kazi za Kila Mwaka 22
Kazi za Mwaka wa Kwanza 22

KIAMBATISHO C – VIWANGO VYA USHURU 23

SHERIA NDOGO 24

Tafsiri: 24

SURA YA KWANZA

1 UTANGULIZI

Kijiji cha Nainokwe kipo katika kata ya Likawage, tarafa ya Nanjirinji wilaya ya Kilwa. Kijiji hiki kipo umbali wa Km 60 kutoka Nangurukuru barabara ya Kibiti-Lindi. Ardhi ya kijiji imepimwa mwaka 2006 ambayo ni hekta 47,980.11. Sehemu kubwa ya ardhi ya kijji imefunikwa na misitu. Msitu wa hifadhi wa kijiji una ukubwa wa hekta 15,966.72.

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 inatoa kipaumbele kwa jami zinazoishi kandokando ya misitu kumiliki na kusimamia misitu. Pia sera inasisitiza mchango wa sekta ya misitu katika kukuza kipato cha jamii ili kupunguza umasikini. Mwaka 2002 serikali ya Tanzania ilipitisha sheria mpya ya misitu Namba 14 ambayo inazipa mamlaka jamii zinazoishi kandokando ya misitu kusimamia misitu yao.

Kijiji cha Nainokwe kimeandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa msitu wa kijiji. Matumizi haya yameanishwa katika mpango huu.

Mpango huu ni mwongozo wa shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha kutumika kwa mpango huu na shughuli hizo zimefafanuliwa na kuwekwa bayana. Shughuli hizo ni uboreshaji wa msitu, kuanzisha utaratibu wa usimamizi, udhibiti wa uvunaji haramu, usimamizi wa sheria za misitu na ukusanyaji na usimamizi wa mapato na matumizi yatokanayo na rasilimali za msitu. Kutakuwa na utunzaji wa kumbukumbu za shughuli zote zilizofanyika ili kuendana na matakwa ya mpango. Kumbukumbu zote zitapatikana pia katika Halmashauri ya Wilaya. Sheria ndogo zitatungwa ili kusimamia utekelezaji wa mpango

Mpango huu umeandaliwa na kamati ya maliasili ya kijiji cha Nainokwe, timu ya wawezeshaji kutoka Halmashauri ya wilaya ya Kilwa chini ya mpango wa usimamizi shirikishi wa msitu kwa kushirikiana na shirika la kuhifadhi mpingo na maendeleo (MCDI). Mpango huu utatumika katika kipindi cha miaka mitano.

1.1 Umiliki wa msitu

Msitu unamilikiwa na Serikali ya Kijiji cha Nainokwe. Msitu wa Kijiji cha Nainokwe ulitengwa kuwa hifadhi mwaka 2009 chini ya usaidizi wa kitaalamu toka kwa wawezeshaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na wawezeshaji wa Shirika la Kuhifadhi Mpingo na maendeleo (MCDI).

1.2 Lengo kuu la ya Mpango wa usimamizi wa misitu

Lengo kuu ni kuweka msitu katika hali ya uasilia na kuboresha hali ya maisha ya kizazi kilichopo na kijacho kwa kutumia rasilimali za misitu kiendelevu.

1.3 Madhumuni

Kuhifadhi eneo lenye ukubwa wa hekta 15,966.72 la Msitu wa Kijiji cha Nainokwe dhidi ya ukataji miti ovyo, uharibifu na matumizi yasiyofaa.

Kuhakikisha kunakuwepo na upatikanaji wa mazao yasiyo timbao kwa wakati wote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kijiji cha Nainokwe kupata mapato kutokana na biashara ya rasilimali za misitu ili kuboresha maisha ya wanajamii wa kijiji.

1.4 Mfumo wa Usimamizi

Usimamizi misitu ya asili unaofuata uvunaji endelevu na upandaji wa miti ya asili kwa kufuata mpango uliopo.

1.5 Muda

Huu ni mpango wa miaka mitano. Mpango huu utarekebishwa na kamati ya maliasili na kupitishwa na halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji mwishoni mwa mwaka wa pili au muda wowote endapo kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Hakutafanyika mabadiliiko yeyote katika mpango huu bila ya kibali cha halmashauri ya wilaya.

SURA YA PILI

2 HISTORIA FUPI YA MPANGO

2.1 Jamii

Kijiji cha Nainokwe kina idadi ya watu wapatao 520 katika kaya zipatazo 120. Kijiji kilisajiliwa tarehe 18/04/1979.

Kijiji hiki kinapakana na kijiji cha Zinga Kibaoni kwa upande wa magharibi, kaskazini ni Msitu wa Hifadhi wa Mitarure; kaskazini mashariki kipo kijiji cha Migeregere na Mavuji, mashariki ni Kijiji cha Liwiti; na upande wa kusini ni Kijiji cha Likawage. Wakazi wa kijiji hiki ni wangindo na Wamwera.

Kijiji hakina Cheti cha Ardhi ya kijiji, Mipaka inajulikana vizuri na kijiji kina muhtasari wa makubaliano kuhusu mipaka pamoja na vijiji vyote vinavyopakana na kijiji cha Nainokwe. Mipaka ya kijiji imewekwa mawe ya kuonyesha mipaka angalia kiambatanisho A, Ramani inayoonyesha mipaka ya kijiji cha Naoinokwe.

Vitongoji vya kijiji ni Nainokwe na Kichonda. Imbinde ni maeneo ya mashamba ambako watu hukaa wakati wa msimu wa kilimo tu (Novemba hadi Juni).

2.1.1 Hali ya Kiuchumi na Kijamii

Wanajamii walio wengi ni wakulima. Wengine hujishughulisha na biashara ndogondogo.

Mazao makuu yanayozalishwa kijijini ni Mpunga, Mahindi, Mtama, Ufuta na Korosho.

Mapato yatokanayo na kilimo kwa kila kaya ni kati ya Shilingi 200,000/- na shilingi 500,000/-kwa mwaka.

Wakulima hujipatia pato la ziada kutokana na ufugaji wa kuku wa kienyeji, ususi wa mikeka na majamvi, migahawa na maduka ya rejareja.

Kila kaya ina idadi ya watu kati ya 4-5.

Huduma za jamii zinazopatikana kijijini ni shule ya msingi, zahanati na visima vya maji na msikiti.

Wananchi huteka maji katika visima vilivyomo ndani ya kijiji.

Mji ulio jirani ni Nangurukuru ambao unafikika kwa miguu masaa 12, baiskeli masaa 5 na kwa gari masaa 3.

2.2 Maelezo kuhusu Msitu

Jina la msitu ni msitu wa Kijawa.

2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake

Msitu wa Hifadhi wa Kijiji cha Nainokwe una ukubwa wa hekta 15,966.72 na upo upande wa magharibi mwa barabara ya Nainokwe-Likawage. Mashamba ya Imbinde yamezungukwa na msitu wa kijiji kwa upande wa magharibi. Msitu wa Kijawa una uoto wa aina tatu: vipande vidogo vya aina ya msitu wa pwani, mbuga zenye miti mifupi na nyasi; misitu ya miombo, na vichaka vizito kandokando mwa mito.

2.2.2 Vyanzo vya Maji

Msitu huu ni chanzo cha maji na hutiririsha maji yake katika;

- Mto Nampekeso ambao humwaga maji yake mto Mtandawala na kuunganisha mto mavuji. Maji yake hutumika katika maeneo ya vijiji vya Liwiti na Mavuji.

Kuna mito ifuatayo katika msitu huu;

- Mto Mtandawala ambao maji yake hutumika katika maeneo ya Liwiti.
- Mto Ligongwe na Namakambale ambayo humwaga maji yake Mto Mtandawala.

2.2.3 Hali ya Udongo

Aina ya udongo katika msitu huu ni Mfinyanzi. Ni udongo unaonata kipindi cha mvua, udongo mwekundu (udongo haugandi umechanganyika na mchanga), Wiwa wa njano na huteleza wakati wa mvua na Kichanga (udongo uliochanganyika na changarawe).

Hali ya kijiografia ya msitu ni tambarare na miinuko kwa maeneo machache

Usawa kutoka baharini ni kati ya mita158 na mita 161

2.2.4 Uoto wa asili na Mazingira.

Eneo hili lina ukanda wa nyasi fupi, miti mifupi aina ya miombo. Kuna vipande vichache vya misitu ya ukanda wa pwani. Kuna aina nyingi za miti baadhi ya miti ya mbao ni michenga, mitondoo, mininga, mmangangwaru, mininga maji, mkongo na mipangapanga. Miti mikubwa ya mininga na mikongo imeshavunwa. Mipingo na mipangapanga nayo ipo lakini uvunaji ulishawahi kufanyika. Misekeseke imekuwa adimu sana kupatikana porini.

2.2.5 Jamii za Miti ya Mbao

Kuna aina nyingi za jamii ya miti katika msitu wa Kijiji. Jamii za miti ya thamani ya mbao zilizopo msituni ni Mninga (*Pterocarpus sp.*), Mkongo (*Afzelia quanzensis*), Mhuba, Mtondoo *(Julbernadia globiflora),* Mpangapanga (*Millettia Stuhlmanii*), Mpingo (*Dalbergia melanoxylon*), Mlomolomo, Mnidu, Msekeseke Mkuruti, Muhamana na Mbonde.

2.2.6 Mazao Yasiyotimbao

Kuna aina mbalimbali za mazao yasiyo timbao kama vile asali ya nyuki wasiouma na wanaouma, uyoga, matundapori, wanyama wadogo, madawa ya asili na kamba.

Miti inayofaa kwa ujenzi ni Mtandawala, Mchenga, Mtondoo na Minepa, Miti ya matunda ni Mgongo, Mtopetope (*Annona sp*), Mfulu, Mkungumwali na mingineyo. Miti inayotumika kutengenezea kamba ni Mchenga (*Jurbenadia globifora*) and Myombo (*Brachystegia spiciformis).*

Jamii za uyoga zifuatazo zinapatikana katika msitu huu Uyogandembo, Nguyugu, Upoa, Uyoga Mbuyu, Ngolowele, Mlelema and Mchinji.

2.2.7 Wanyama Pori na Jamii za Mimea

Kuna aina mbalimbali za wanyapori na jamii mbalimbali za mime zinazopatikana katika msitu huu. Wanyama hawa ni kama Kinyonga asiye na mkia (Nakatoga), Paa, Ngiri/nguruwe, Tembo na Chatu. Pia kuna aina mbalimbali za ndege.

2.3 Maeneo Madogo ya Usimamizi (EDU)

Msitu huu umegawanyika katika maeneo madogo mawili ya usimamizi kutokana na tofauti kubwa katika aina za uoto. Eneo lenye ukubwa wa hekari 8,502 lina uoto wa miombo iliyofunga pia kuna miti mikubwa. Eneo la hekari 7,465 ni vichaka kwa wingi, nyasi na miti midogo.

Eneo la asilimia 10 ya msitu limetengwa kama eneo lisilovunwa na uvunaji wa mazao ya misitu hauruhusiwi kabisa katika eneo hili. Eneo hili limeonyeshwa katika kiambatisho A

kwenye ramani ya msitu wa Kijiji. Eneo hili limetengwa kutokana na kuwa na sifa ya misitu ya pwani. Eneo hili ni hifadhi ya wanyama wakati wa kiangazi kwa kuwa haliungui moto kwa urahisi.

2.4 Matumizi ya Msitu

Katika msitu huu, uvunaji wa miti ya mbao aina mbalimbali ulifanyika kwa kipindi kilichopita. kwa sasa uvunaji utafanyika kwa kufuata mpango wa uvunaji.

2.4.1 Mambo ya Asili na Haki za Kijadi

Kuna eneo ndani ya msitu wa Hifadhi liitwalo Imbinde Kibanda cha Ngolyo ambalo wanajamii hufanyia matambiko. Wanajamiii watakuwa na haki ya kuendeleza shughuli za kijadi kwa kutoa taarifa kwa uongozi unaohusika na usimamizi wa msitu.

2.4.2 Historia ya Nyuma

Eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya uhifadhi wa msitu lilikuwa na tatizo kubwa la uvunaji haramu wa magogo. Pia uvunaji halali ulifanyika pamoja na uwindaji wa wanyama.

2.4.3 Matumizi ya sasa

Uwindaji wa kitalii ambao hufanywa na wageni katika maeneo ya nyasi fupi uvunaji waimajengo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba . Wanakijiji hutumia mitego na kuwashambulia wanyama pale wanapozama kwenye matope wakati wa kiangazi hasa maeneo ya Matanda Mawili.

SURA YA TATU

3 MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU

Vipengele katika sura hii vinaweka bayana taratibu za kuingia msituni na za matumizi ya mazao ya msitu.

3.1 Matumizi ya msingi

Wanajamii wa kijiji cha Nainokwe watakuwa na haki ya kuingia katika msitu wa jamii bila kibali kupata matumizi ya msingi ya kufanya matambiko, maji na kupita njia zinazofahamika, haki hii itahusu vijiji jirani pia.

3.2 Matumizi huru ya msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Nainokwe yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao, asali ya nyuki uyoga, kuni, majengo, matundapori, madawa asili na kutundika mizinga, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure kutoka serikali ya kijiji.

Wasio wakazi wa kijiji cha Nainokwe wanaweza pia kuomba kibali toka serikali ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu toka msitu wa kijiji. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao ya msitu ya bure yanatumika kiendelevu.

3.3 Shughuli katika msitu zitakazotozwa ushuru

Shughuli zifuatazo zitatozwa ushuru na serikali ya kijiji.

- Kutembelea msitu kwa ajili ya mafunzo.
- Utafiti.
- Utalii msituni.

Watalaam na wawezeshaji hawatahusika na kutozwa ushuru. Viwango vya ushuru vimeonyeshwa katika kiambatisho C

3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji

3.4.1 Utaratibu wa kupata vibali ya uvunaji miti ya mbao

Utaratibu huu utahusisha miti yote iliyoorodheshwa katika kipengele 2.2.5 hapo juu.

- Mtu yeyote anayetaka kuvuna mazao ya misitu toka Msitu wa Kijiji lazima kwanza aandike barua ya maombi kijijini na aonyeshe aina na kiasi anachotarajia kuvuna.
- Serikali ya kijiji ikishirikiana na kamati ya Maliasili itajadili na kupitisha ombi hilo endapo itaridhia kufuatana na matakwa ya mpango wa usimamizi na mpango wa uvunaji. Kama mpango wa uvunaji haujaandaliwa kibali hakitatolewa na uvunaji hauruhusiwi.
- Kama haijaainishwa katika mpango wa uvunaji, Kamati ya Maliasili itapanga bei ya kuvuna mazao ya misitu na bei hizo kupitishwa na Serikali ya Kijiji.
- Mwombaji atalipa gharama za leseni kwa Kamati ya Maliasili na kupatiwa stakabadhi halali ya malipo.
- Mwombaji atawasilisha stakabadhi ya malipo kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atampatia leseni ya kuingia msituni na kuvuna zao lililokubaliwa.

- Mwombaji atarudi tena kijijini na kuwasilisha leseni kijijini, Kamati ya Maliasili itamwonyesha eneo la kuvuna mazao ya misitu anayoyahitaji.
- Baada ya kuvuna magogo yote yaliyokatwa na visiki yatagongwa nyundo iliyokubalika.
- Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha kusafirishia toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya ili aweze kusafirsha mazao yake bila usumbufu nje ya Wilaya.
- Kibali hiki hutolewa kwa ada na Afisa misitu wa wilaya na lazima kiwasilishwe kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji ambaye ataweka kumbukumbu ya nambari ya kibali kabla mzigo haujatolewa kijijini.

3.4.2 Mazao mengine ya misitu yatokanayo na leseni

Mazao mengine yote yatalipiwa ushuru sawa na sheria ndogo ya kijiji husika ila ada hiyo isizidi viwango vya sheria mama.

3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Uvunaji wa miti ya mbao ambayo haijaorodheshwa katika kipengele 2.2.5 hapo juu au miti ambayo haijatengenezewa mpango wa uvunaji. Kilimo ndani ya msitu
- Makazi ndani ya msitu
- Kuchoma moto ovyo
- Kuchoma moto bila kibali

SURA YA NNE

4 HAKI, MANUFAA NA MAJUKUMU YA WADAU

Msitu wa kijiji cha Nainokwe una wadau wafuatao; Halmashauri ya Kijiji, Kamati ya Maliasili, wanakijiji, Halimashauri ya Wilaya ya Kilwa, serikali kuu na wadau wengine. Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

4.1 Kijiji

4.1.1 Haki

- Kumiliki na kutunza msitu wa Kijiji.
- Kukamata, kupiga faini au kumshitaki mtu yeyote anayeenda kinyume na sheria ndogo za kijiji zilizopitishwa na mpango huu.
- Kutumia rasilimali kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii na hivyo kuboresha hali za maisha ya wanajamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya msitu.

4.1.2 Manufaa

- Kutumia mazao ya misitu bila mashariti magumu kama ilivyoainishwa katika mpango wa usimamizi misitu.
- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa huduma za jamii kijijini.
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu ni mali ya kijiji ingawa kunaweza kuwa na makubaliano ambapo Halmashauri ya Wilaya itapata gawio fulani kutokana na huduma za uwezeshaji kama ilivyobainishwa katika kipengele 7.2.
- Kupata mafunzo ya kitaalam katika masuala mbalimbali ya usimamizi misitu na kuboresha maisha ya jamii.

4.1.3 Majukumu ya Halmashauri Kijiji

- Msimamizi mkuu wa shughuliu zote za utunzaji wa msitu.
- Kuthibiti mapato na matumizi yote yatokanayo na msitu.
- Kutatua migogoro inayohusiana na misitu pale inapojitokeza na kupeleka matatizo hayo ngazi ya Halmashauri ya Wilaya pale yanaposhindikana kutatua.
- Kudhibiti uvunjwaji wa sheria.
- Kuhakiki vibali vyote vilivyotolewa na Kamati ya Maliasili.
- Kupokea taarifa za uharibifu wa msitu toka Kamati ya Maliasili na wanakijiji kwa ujumla na kuzifanyia kazi.
- Kujadili na kupitisha mipangokazi ya mwaka ya Msitu wa Kijiji iliyoandaliwa na kamati ya Maliasili.

- Kujadili na kuidhinisha matumizi yote ya fedha kwa kamati ya Maliasili, doria,na wajumbe wa serikali ya kijiji kwa ajili ya shughuli za msitu.

4.1.4 Majukumu ya Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za msitu kama vile; upandaji miti, ukusanyaji wa mazao ya misitu na kutunza kumbukumbu za msitu.
- Kutoa vibali vilivyoruhusiwa vya uvunaji wa mazao ya misitu
- Kuhakikisha doria imefanyika kila mara na kwa uhakika.
- Kuandaa mpango kazi wa mwaka wa shughuli za msitu.
- Kutathimini rasilimali za misitu na kutengeneza mpango wa uvunaji
- Kutoa taarifa za maendeleo na uharibifu wa msitu kwa Halmashauri ya kijiji.
- Kusimamia na kufuatilia uvunaji.
- Kuratibu shughuli zote zinazofanyika msituni
- Kupendekeza na kusimamia sheria ndogoikiwemo kuzirekebisha inapohitajika.
- Kuijulisha jamii juu ya matukio katika Msitu wa Kijiji na maeneo yanayozunguka.
- Kuielimisha jamii juu ya mabadiliko ya miongozo mbalimbali ya utunzaji misitu.
- Kubuni maeneo zaidi ya kuhifadhi
- Kutoa tarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa misitu kwa Afisa Misitu wa Wilaya.
- Kutoa tarifa ya robo mwaka kwa Halmashauri ili kuendana na utaratibu mpya wa kuweka kumbukumbu.utaratibu huu unajulikana kwa kitaalam kama NAFOBEDA.

4.1.5 Majukumu ya Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika msitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya misitu.
- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya msitu kwa Kamati ya Maliasili na Halmashauri ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha msitu.
- Kupitia na kuidhinisha sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika kulinda msitu na kutoa msaada kwa timu ya doria mara kwa mara.
- Kushiriki kwa dhati katika kuzima moto..

4.2 Halmashauri ya Wilaya

4.2.1 Haki

- Kupokea taarifa za mara kwa mara juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa msitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.

- Kuchukua tena mamlaka ya usimamizi wa msitu chini ya halmashauri ya wilaya kama kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo.

4.2.2 Manufaa

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa misitu.
- Kuboreka kwa usimamizi wa misitu.
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii.

4.2.3 Majukumu

- Kutoa wataalam kwa ajili ya shughuli za msitu pale inapohitajika.
- Kusaidia kutafuta soko bora la mazao ya misitu.
- Kusimamia na kutatua migogoro ambayo iko juu ya uwezo wa serikali ya kijiji.
- Kuongoza zoezi la kubaini fursa na vikwazo katika kipindi cha kwanza na cha mwisho cha mpango huu.
- Kuingilia kati kama kuna jambo au shughuli yeyote imefanyika kinyume cha utaratibu wa mpango.

4.3 Serikali Kuu

4.3.1 Majukumu

- Kutoa wataalam, washauri pale wanapohitajika.
- Kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.

SURA YA TANO

5 SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Mikakati ya jumla ya kutunza na kuendeleza misitu pamoja na rasilimali zake imewekwa bayana. Mambo yatakayoangaliwa ni utunzaji wa misitu hii ili isiharibiwe dhidi ya kilimo na moto. Ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mpango wa matumizi endelevu wa mazao ya msitu utazingatiwa.

5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu.

Katika kuendeleza msitu, mikakati ya jumla itakayofanyika ndani ya msitu ni kama ifuatavyo:-

- Kuthibiti aina yoyote ya kilimo ndani ya msitu.
- Kuthibiti uchomaji moto ovyo msituni.
- Kufanya doria za mara kwa mara ili kuthibiti ukataji holela wa miti na uharibifu mwingine wa msitu.

5.2 Ulinzi wa msitu

5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu.

Usimamizi wa msitu wa kijiji utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii wote. Msitu utalindwa na jamii kuzingatia mipaka yake, kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

5.2.2 Walinzi wa doria

Kutakuwa na timu ya doria itakayochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji ambayo itakuwa na jukumu la kufanya doria za mara kwa mara katika msitu wa jamii.

5.3 Kusafisha Mpaka na Barabara za Kuzuia Moto

Kamati ya maliasili ya kijiji na jamii kwa ujumla watashiriki katika kusafisha mpaka wa msitu na kutengeneza barabara za kuzuia moto. Kamati ya maliasili itaamua wapi barabara za kuzuia moto zipite baada ya kupata ushauri toka kwa Afisa Misitu wa Wilaya. Ubabuaji moto ni hatua mojawapo muhimu katika kuthibiti moto, na hili ni jukumu la kamati ya maliasili na wanajamii kwa ujumla. Zoezi la ubabuaji na usafishaji wa barabara za moto ni kazi ngumu inayohitaji fedha toka vyanzo mbalimbali.

SURA YA SITA

6 MAPATO NA USIMAMIZI WA MAZAO YA MSITU

6.1 Vyanzo vya mapato

Kutakuwa na vyanzo vya mapato vifuatavyo toka msitu wa jamii:

- Ada za vikundi vilivyoko mafunzoni, shughuli za utafiti na utalii
- Faini za wahalifu
- Ushuru
- Ada za leseni
- Na mengineyo

6.2 Mgawanyo wa Mapato kwa Wadau

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao ya msitu utakuwa kati ya serikali ya kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kutunza na kuendeleza msitu. Halmashauri ya wilaya watapewa asilimia 5 ya mapato ya msitu, kijiji asilimia 45 na kamati ya maliasili asilimia 50. Kila mwaka Serikali ya kijiji itatoa kiasi fulani cha mapato yatokanayo na rasilimali za misitu kwa Halmashauri ya Wilaya kulingana na huduma ambazo Halmashauri imetoa.

6.3 Matumizi ya mapato

Mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za;

- Kuendeleza shughuli za msitu zilizopangwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Mapato yatakayobaki yatapelekwa kwa serikali ya kijiji ili yatumike katika shughuli za jamii.

Matumizi halali ya mapato yatokanayo na msitu wa jamii ni:

- Kulipa motisha (posho) kwa doria.
- Vifaa muhimu kwa ajili ya kuendeleza shughuli za msitu kama ilivyobainishwa katika mpango kazi wa mwaka.
- Matumizi mengine ya ziada ya kuendeleza msitu yaliyoidhinishwa na Serikali ya Kijiji.
- Ununuzi wa vitabu kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za shughuli za msitu.
- Kuchangia katika shughuli za maendeleo kijijini.

6.4 Ukusanyaji na utunzaji wa Fedha

Fedha zote za kamati ya maliasili zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi kidogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi 50,000/=. Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la **Akaunti ya Maliasili ya Kijiji cha Nainokwe** na itakuwa na watia sahihi wafuatao; Afisa Mtendaji wa Kijiji (A), Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mipango ya Kijiji (B), Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili (A) na mweka Hazina (B) wa Kamati ya Maliasili ya kijiji. Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

6.4.1 Vitabu muhimu vya kutunza kumbukumbu vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu. Vitabu vinatakiwa kuwa tayari kwa ukaguzi wakati wowote na vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya serikali ya kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/imuhtasa wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria kinachoonyesha tarehe ya doria, njia iliyotumika, kama kuna wahalifu waliokamatwa na dalili zozote za kuwepo kwa uharibifu wa msitu.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu kinachoonyesha majina ya wahalifu, faini zilizolipwa, tarehe na nambari ya stakabadhi.
- Vitabu vya vibali na leseni vinavyoonyesha nambari ya kibali, mpewaji, sababu ya kibali, kiasi cha mzigo, kiasi cha fedha, nambari ya stakabadhi, tarehe na jina la mwanakamati aliyesimamia.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango kazi huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.

6.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Kamati ya maliasili itatoa taarifa ya mapato na Matumizi kila mwezi kwa serikali ya kijiji na kila baada ya miezi mitatu kwa mkutano mkuu wa kijiji.

6.4.3 Kuwajibishwa

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluhishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na nafasi iliyoacha wazi ijazwe kufuata utaratibu unaokubalika.

SURA YA SABA

7 UFUATILIAJI NA TATHIMINI

7.1 Ufuatiliaji

Serikali ya Kijiji itafuatilia shughuli zote zilizopangwa kulingana na mpango kazi wa kila mwaka katika kipindi chote cha miaka mitano. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli zote zimefanyika kulingana na mpango kazi.

7.2 Tathimini ya kati na ya mwisho

Zoezi la kubaini fursa na vikwazo litafanyika ili kuelewa hali ya maendeleo kama ilivyobainishwa katika mpango kazi huu. Zoezi hili litafanyika mwishoni mwa mwaka wa pili.

UHALALI WA MPANGO

Mpango wa Usimamizi Misitu

Mpango huu wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Kijiji cha Nainokwe umepitishwa na mkutano mkuu wa kijiji, Baraza la maendeleo la Kata na Baraza la madiwani.

Mpango huu unasisitiza kuwa ni jukumu la wanakijiji wa Nainokwe kutunza, kusimamia, kutumia kiendelevu na kuendeleza msituwetu kufuatana na malengo ya mpango huu.

Marekebisho ya Mpango

Jamii ya kijiji cha Nainokwe haitafanya marekebisho ya jambo lolote katika mpango huu bila kuomba ushauri kwa Afisa Misitu wa Wilaya ambaye atashauri na kutoa maoni juu ya marekebisho hayo. Marekebisho hayo yakikubaliwa yatatiwa saini na yataambatanishwa katika mpango huu. Kwa madhumuni ya ufanisi wa haraka wa marekebisho hayo, Afisa misitu wa Wilaya anaweza kutia sahihi kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya.

Mpango huu wa usimamizi wa msitu wa kijiji cha Nainokwe umesainiwa na:

_____	_____
Mwenyekiti wa Kijiji	Mwenyekiti Kamati ya Maliasili
Kwa niaba ya Jamii ya kijiji cha Nainokwe	Kwa niaba ya Kamati ya Maliasili
Tarehe……..	Tarehe……..

_____

Mustafa Mufangavo

Afisa Misitu Wilaya

Tarehe……

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A – RAMANI YA MSITU WA KIJIJI

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Kijiji



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Kijiji cha Nainokwe. Vijiji vinavyopakana na Nainokwe vimeonyeshwa, mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu duara na kupewa nambari. Vipimo vya GPS (UTM37S : Arc 1960) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1	SR604	513396	9008074
2	SR616	519041	9006717
3	UCHUNGWA	520500	9001900
4	SR614	510696	8993612
5	SR606	507617	8989514
6	SR613	504777	8984428
7	SR612	502645	8984680
8	SR611	486045	8979258
9	SR605	481588	8993178
10	SR607	484275	9000796
11	SR608	492967	8997796
12	SR609	503821	8994412
13	SR610	505907	8995006

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
14	SR615	505197	8996206

Ramani Awali inayoonyesha Matumizi ya Ardhi ya Kijiji

Ramani hii iliandikwa na wanakijiji wa Nainokwe.

Ramani inayoonyesha Mipaka ya Msitu wa Kijiji



Ramani hapo juu inayoonyesha mipaka ya Msitu wa Kijiji cha Nainokwe. Mawe ya mipaka yameonyeshwa kwa alama ya pembetatu na kupewa nambari. Eneo linaloonekana jeusi ni eneo la uhifadhi ambapo uvunaji hauruhusiwi kabisa. Vipimo vya GPS (UTM37S : Arc 1960) katika mawe ya mipaka ni kama ifuatavyo;

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
1		499344	8995629
2	SR609	503915	8994204
3	SR610	506001	8994798
4		505711	8992751
5		503875	8992555
6		503515	8991664
7		504289	8990393
8		504447	8989598
9		503795	8987782
10		503422	8986501
11		503151	8985571
12	SR612	502739	8984473
13		495738	8982187
14		495379	8984060
15		494698	8986538

Namba	Nambari ya utambulisho	E (m)	N (m)
16		490813	8985479
17		489093	8984798
18		486806	8984877
19		484275	8984872
20	SR605	481683	8992971
21		495135	8990379
22		497649	8989895
23		498788	8989676
24		499002	8990099
25		499247	8990584
26		498961	8992135
27		498576	8994226
28		499907	8990375
29		500201	8990287
30		500462	8990306
31		501104	8989877
32		502748	8989592
33		499825	8987472
34		497978	8988083

Ramani ya Usawa kutoka Baharini ya Msitu wa Kijiji



Sehemu inayoonyesha weupe ni maeneo ya miinuko na sehemu nyeusi ni maeneo ya mabondeni

Ramani Shirikishi ya Msitu wa Kijiji

Ramani hii iliandikwa na wanakijiji wa Nainokwe.

KIAMBATISHO B : MPANGO WA UTEKELEZAJI

Kila mwaka kamati ya maliasili ya kijiji ni lazima iandae mpango kazi kwa mwaka unaofuata.

Kazi za Kila Mwaka

- Doria za mara kwa mara
- Kubabua
- Kusimamia matumizi ya sheria ndogo (Serikali ya Kijiji)
- Kuweka kinga za moto (Kamati ya maliasili)
- Kuweka barabara za moto (Wanajamii/Kamati ya Maliasili)
- Ulinzi wa Msitu (jamii nzima)
- Kukusanya mapato yatokanayo na mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)

Kazi za Mwaka wa Kwanza

- Kusafisha mipaka kuzunguka msitu (Jamii na Kamati ya maliasili)

- Kujenga kituo cha ukaguzi wa mazao ya misitu (Kamati ya maliasili)

KIAMBATISHO C – VIWANGO VYA USHURU

- Makundi ya mafunzo yatakayotembelea msitu yatatozwa shilingi zisizozidi 10,000/- kwa kikundi
- Watafiti kila mmoja atalipa shilingi zisizozidi 3,000/- na taarifa ya utafiti kurudi kijijini.
- Watalii watalipa shilingi 5,000/- kwa siku kwa kichwa. Waongoza watalii na wageni watalipwa shilingi 2,000/- kwa siku kwa kichwa. Watalii watanzania watatozwa shilingi 1,000/= kwa kichwa kwa siku.

SHERIA NDOGO

SHERIA NDOGO ZA KUTUNZA, KUSIMAMIA NA KUTUMIA RASILIMALI ZA MISITU YA JAMII KATIKA KIJIJI CHA NAINOKWE.

Sheria hizi zimetungwa chini ya kifungu cha 120 (1) na 163 cha Sheria za serikali za mitaa ya mwaka 1982 Na. 7 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2000

Jina: Sheria hizi zitaitwa sheria za kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za misitu ya jamii katika kijiji cha Nainokwe

Tarehe: Sheria hizi zitaanza kutumika kuanzia tarehe ……

Tafsiri:

Msitu wa Kijiji: Maana yake ni eneo la msitu lililotengwa na kijiji lenye miti na uoto mwingine wa asili linalomilikiwa na kijiji cha Nainokwe.

Mpango wa Usimamizi wa Misitu: Maana yake ni kabrasha lenye maelezo ya namna jamii ya kijiji cha Nainokwe itakavyotunza, kusimamia na kutumia rasilimali za msitu.

Halmashauri ya kijiji: Maana yake ni wajumbe 25 wa Halmashauri ya serikali ya kijiji cha Nainokwe.

Mkutano mkuu wa Kijiji: Maana yake ni Mkutano wa wananchi wote wa kijiji cha Nainokwe wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho katika kijiji cha Nainokwe kinachohudhuriwa na wanakijiji wote wenye akili timamu na wenye umri usiopungua miaka 18.

Kamati ya Maliasili ya Kijiji: Maana yake ni kamati iliyochaguliwa na kuundwa na serikali ya kijiji kupitia mkutano mkuu wa kijiji cha Nainokwe ambayo majukumu yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu misitu iliyopo ndani ya mipaka ya kijiji na maliasili nyingine zilizomo kwenye kijiji cha Nainokwe.

Meneja wa Msitu: Maana yake ni kamati ya maliasili ya kijiji ambayo kazi yake ni kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu msitu.

Mwanakijiji: Maana yake ni mtu yeyote aliyeandikishwa na serikali ya kijiji cha Nainokwe kuwa mwanakijiji wa kijiji cha Nainokwe.

Kijiji: Maana yake ni kijiji cha Nainokwe pamoja na vitongoji vyote vinne

Kiongozi: Mtu yeyote aliyepewa madaraka na mamlaka na wananchi ili awatumikie

Sehemu A: Sheria Ndogo

Sheria Na. 1: Utaratibu wa jumla wa kutumia msitu na mazao ya msitu.

Watu ambao wanaruhusiwa kuingia katika misitu ya kijiji kwa shughuli mbalimbali za usimamizi kutokana na taratibu zilizokubalika ni wakazi wa kijiji cha Nainokwe tu.

Watu wengine kutoka nje ya kijiji cha Nainokwe wataruhusiwa kuingia ndani ya misitu hii kwa vibali maalum endapo watakuwa na shughuli iliyokubalika.

Kwa wale wanakijiji wasiojiweza ambao wanatambuliwa na serikali ya kijiji kama vile wagonjwa wa kudumu, walemavu na wazee watachukua mazao ya msitu yasiyo ya biashara bure bila kutozwa ushuru wa aina yeyote.

Kwa mazao madogomadogo ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama vile uyoga, matundapori, mbogamboga, kuni, madawa na ukindu hapatakuwa na malipo ila kutakuwa na siku maalum ya kukusanya mazao hayo siku hiyo inaweza kubadilika kutokana na matakwa ya jamii.

Mazao yote ambayo ni kwa ajili ya biashara yatavunwa kwa kulipia ushuru.

Sheria Na. 2: Masharti ya matumizi ya msitu na mazao ya msitu wa jamii.

(i) Matumizi yaliyoruhusiwa bila kibali wala ushuru/ada:

- Njia za miguu
- Kuokota kuni kavu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani
- Uyoga, matundapori, mbogapori na madawa ya asili kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

(ii) Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kibali maalum:

- Kutundika mizinga na uvunaji wa asali.
- Kuchimba mabwawa ya samaki sehemu zenye maji ndani ya msitu.
- Kutumia mazao ya misitu kwa ajili ya maendeleo ya huduma za jamii kama vile ukaarabati/ujenzi wa shule, hospitali n.k.

(iii) Matumizi yaliyoruhusiwa kwa kulipiwa ushuru/ada

- Miti ya majengo
- Kuwinda wanyamapori
- Kuwinda ndege.
- Kuvuna magogo.
- Kuingia ndani ya msitu kwa ajili ya kufanya utafiti, mafunzo, au utalii.
- Kuchunga mifugo isipokuwa mbuzi.
- Kuvuna mazao yaliyotajwa kwenye kipengele c na d hapo juu kwa ajili ya biashara.

(iv) Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Kuchoma moto ovyo msituni
- Kukata na kupasua miti ya mbao iliyozuiliwa
- Kutega wanyamapori ambao si waharibifu wa mazao ya kilimo.
- Kuharibu uoto wa asili sehemu yeyote katika msitu.
- Kuvuna asali kwa kutumia moto.
- Shughuli za kilimo.
- Makazi ya watu.
- Kuchoma mkaa.

Sehemu B: Adhabu

VIWANGO VYA ADHABU NA FAINI

Adhabu na faini

(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote ambaye bila ya kibali au idhini yoyote ya kisheria akitiwa hatiani na sheria hii kwa kutenda mojawapo ya kosa au shughuli iliyopigwa marufuku katika msitu ikiwa ni pamoja na kukiuka taratibu za matumizi ya msitu kwa shughuli zinazotolewa kibali au taratibu nyingine zilizowekwa na sheria hii.

(a) Kulima, kutega wanyama, kuweka makazi au kuchoma msitu faini shilingi 20,000/= au kufikishwa mahakamani
(b) Kupatikana na magogo, mbao au nguzo bila ya kibali faini shilingi 50,000/= au kufikishwa mahakamani.
(c) Kuwinda wanyama au kuchoma mkaa ndani ya msitu bila ya kibali faini shilingi 20,000/=
(d) Kuondoa au kubadili alama za msitu faini shilingi 20,000/=
(e) Kuchimba mawe ndani ya msitu bila ya kibali faini shilingi 10,000/=
(f) Kurina asali kwenye mapango ya miti au kwenye mashimo ardhini faini shilingi 8,000/=
(g) Kuingia msituni, kukata kuni mbichi, kuchuna magome ya miti, kupatikana na vifaa vya uvunaji ndani ya msitu au kwa shughuli za biashara kuchukua dawa za tiba, matunda, miyaa, ukindu, uyoga, fito, kongowele, udongo, nyasi, miswaki, pikicho au mboga faini kwa kila kosa shs 5,000/=
(h) Kuchunga mifugo ndani ya msitu bila ya kibali faini kwa kila mnyama shilingi 2,000/=
(2) Kiongozi akipatikana na hatia ya kuhusika katika kukiuka mojawapo ya taratibu zilizowekwa na sheria hii faini yake ni shilingi 20,000/= pamoja na faini ya kosa alilotenda.
(3) Mtu yoyote ambaye atapuuzia au kukataa kutoa faini, vifaa au rasilimali aliyokamatwa nayo au kukataa kujaza fomu ya kukiri kosa ikiwa ni pamoja na kurudia kosa atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma.
(4) Nyara zote zitakazokamatwa kutokana na makosa yaliyotajwa (a-i) zitataifishwa na kuuzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kufuata taratibu zilizowekwa na serikali na fedha zitakazopatikana zitakuwa mali ya kijiji.Sheria hii imepitishwa kwenye Baraza la Madiwani la Tarehe …….. na kusainiwa na:

…….. ……

Mh. Ally Mohamed Mtopa **Amiri Gwakirayi**

Mwenyekiti wa Halmashuri (W) Mtendaji (W) **Mkurugenzi**

…….
…….

Tarehe Tarehe